Liturgia

SHANGWE NA SIFA

Wimbo waweza kuimbwa wakati wahudumu wakielekea madhabahuni.
Watu wakiwa wamesimama mhudumu aseme

Mhudumu:
Ahimidiwe Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu
Waumini:
Ubarikiwe ufalme wake sasa na hata milele. Amina

Wakati wa pasaka hadi pentekote maneno haya yasemwe badala ya hapo juu

Mhudumu:
Haleluya! Kristo amefufuka
Waumini:
Bwana amefufuka kwelikweli ! Haleluya

Wakati wa majilio, mafungo, na vipindi zingine za toba:

Mhudumu:
Ahimidiwe Bwana awezae kutusamehe dhambi zetu zote
Waumini:
Kwa maana fadhili zake ni za milele

Mhudumu anaweza kuomba

Mwenye zi Mungu, ambaye mioyo yote i wazi kwako na mahitaji yote hujulikana, wewe ambaye kwako hakuna siri iliyofichika: utakase mawazo ya mioyo yetu kwa uwezo wa Roho wako Mtakatifu ili tukupende kwa kweli na kuliinua kwa uthamani jina lako takatifu; kwa Kristo Bwana wetu. Amina.

UFUPISHO WA AMRI

Yesu alisema,"na amri ya kwanza ndiyo hii: Sikia Ee! Israel, Bwana Mungu wetu ni Mungu mmoja. Utampenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. Hii ndiyo amri ya kwanza na ya pili yafanana nayo nayo ni hii: Umpende jirani yako kama nafsi yako: hakuna amri liyo kuu kama hii."

Moja ya taratibu ya kyrie (Bwana Utuhurumie) yaweza kusemwa au kuibwa

Bwana Utuhurumie
Kristo utuhurumie
Bwana utuhurumie

Au
Mungu Mtakatifu, Mtakatifu mwenye enzi
Mtakatifu usiyekufa,
Utuhurumie

Wote na wasimame kuimba au kusema wimbo ufuatao: Utukufu huachwa wakati wa Majilio na Mafungo.

UTUKUFU UNA MUNGU JUU MBINGUNI

Utukufu una Mungu juu mbinguni, na amani duniani kwa watu wake.

Bwana Mungu, mfalme wa mbinguni, mwenye enzi Mungu Baba, tunakuabudu wewe, tunakushukuru wewe, tunakusifu wewe kwa ajili ya utukufu wako.

Bwana wetu Yesu Kristo, Mwana pekee wa Baba, Bwana Mungu, Mwana kondoo wa Mungu, uchukuaye dhambi za ulimwengu: Uturehemu; uketiye mkono wa kuume wa Baba: Upokee maombi yetu.

Kwa maana wewe pekee ndiye mtakatifu, wewe pekee ndiwe Bwana, wewe pekee uliye Juu Sana, Yesu Kristo, pamoja na Roho Mtakatifu, kwa utukufu wa Mungu Baba. Amina.

KUSIFU NA KUSUJUDU

Hapa kinafuata kipindi cha sifa. Kipindi hiki kinategemewa kufuatiwa na vipindi vya nyimbo katika ulimwengu wa Roho, Unabii, kunena kwa lugha na kutafsiri kama Roho Mtakatifu atakavyoongoza. Baada ya kipindi hiki, Ibada itaendelea kwa maongozi ya Mhudumu.

SALA YA SIKU

Mhudumu aseme kwa watu:

Mhudumu: Bwana awe nanyi
Waumini: Awe pia na roho yako
Mhudumu: Na tuombe

Sala ya siku iliyochaguliwa inatolewa hapa

Waumini: **Amina**

NENO LA MUNGU

Watu na wakae. Msomaji aliyechaguliwa atasoma neno, akianza kwa kusema:

Somo kutoka _____
Somo, sura, na mstari vinaweza kuongezwa hapa

Baada ya somo, msomaje anaweza kusema:

Msomaji: Hili ndilo neno la Mungu
Waumini: Tumshukuru Mungu

SOMO KUTOKA AGANO LA KALE

ZABURI

WARAKA

INJILI TAKATIFU

Watu wote wakiwa wamesimama, Shemasi au ka atasoma Injili, akisema

Shemasi: Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo ☋ kama ilivyoandikwa na mtakatifu_____

Wakati maneno hayo juu yakinenwa, watu waweza kufanya alama ya msalaba kwenye kipaji cha uso, mdomo, na kwenye moyo, na halafu waitikie kwa kusema:

Waumini: Utukufu ni kwako wewe, Bwana Yesu Kristo.

Baada ya Injili, shemasi anasema

Shemasi: Injili ya Bwana
Waumini: Sifa ni kwako ee Bwana Yesu Kristo

MAHUBIRI

IMANI YA NIKEA

(Inakubalika kuinama kabisa wakati vipengere vilivyopigiwa mistari vikisemwa)

Tunamwamini Mungu mmoja, Baba, Mwenye zi,
Muumba mbingu na nchi, na vitu vyote vanavyoonekana na visivyoonekana.

Tunamwamini Mungu mmoja, Yesu Kristo, Mwana pekee wa Baba, mwana wa milele yeye asiyeumbwa, Nuru kutoka katika Nuru , Mungu ktoka katika Mungu, Mungu kweli kutoka katika Mungu kweli, mzaliwa ambaye hakuumbwa. Yeye ambaye ni mmoja na Baba. Katika yeye vitu vyote viliumbwa.

Yeye aliyeshuka kutoka mbinguni kwa ajili yetu na kwa wokovu wetu Alitungwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, akazaliwa na bikira Mariamu, Akafanywa kuwa binadamu. Alisulubiwa kwa ajili yetu zamani za pontio pilato Aliteswa, akafa, akazikwa.

Siku ya tatu akakafufuka, kama yanenavyo maandiko matakatifu, akapaa mbinguni, ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba. Atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio hai na walio kufa. Na ufalme wake hautakuwa na mwisho
Tunamwamini Roho Mtakatifu, Bwana, mtoa uzima,
Yeye atokaye katika Baba na Mwana
Yeye anayeabudiwa na kutukuzwa pamoja na baba na mwana
Yeye aliyenenwa kwa vinywa vya manabii
Tunaamini kanisa moja Katoliko na Apostoliko
Tunatambua ubatizo mmoja wa ondoleo la dhambi
Tunatazamia kufufuliwa kwa wafu ☋ na uzima wa ulimwengu ujao. Amina.

MAOMBI KWA AJILI YA WATU

Kiongozi na watu wataomba kwa kupokezana

Taratibu ya kwanza ya maombi 1

Baba, tunaombea kanisa lako takatifu katoliko;
= Ili wote tuwe na umoja=

Ujalie kwamba kila muumini wa kanisa lako akutumikie wewe kwa unyenyekevu wake wote.
= Ili watu wote walitukuze jina lako

Tunaomba kwa ajili ya Maaskofu wote, Makasisi na Mashemasi.
= Ili wawe wahudumu waaminifu wa neno lako na sakramenti yako=

Tunaomba kwa ajili ya watawala wote na wenye mamlaka katika mataifa ya dunia
= Ili kuwe na haki na amani duniani kote

Tupe neema ya kufanya mapenzi yako katika yote tuyafanyayo
=Ili kazi ya mikono yetu ipate kibali machoni pako

Uwaangalie kwa rehema zako wote wanaoteseka kwa huzuni au matatizo mbalimbali;
= Ili waondokane na shida zao

Uwapumzishe kwa amani ya milele wote waliofari ki dunia
=Na uwaangazie nuru yako isiyo na kikomo

Tunakusifu kwa ajili ya watakatifu wako walioingia katika furaha;
=Tujalie nasi tuje kushiriki katika ufalme wa mbinguni

Na tuombe kwa ajili ya shida zetu pamoja na za wengine.

Waumini wanakaribishwa kuongeza mahitaji yao binafsi
Mhudumu anaongeza na kumalizia sala ya siku

Taratibu ya maombi II

Kwa Amani , tunaleta sala zetu kwako wewe, Bwana Mungu

Kimya
Kwa ajili ya watu wote katika maisha yao na kazi zao za kila siku
= Kwa ajili ya familia zetu, marafiki zetu, na majirani zetu na hao wenye upweke=

Kwa ajili ya jumuia hii, taifa hili, pamoja na dunia yote;
=Kwa wote wafanyao kazi kwa ajili kutetea haki, uhuru, na amani=

Kwa ajili haki na matumizi mema ya maumbile yako
=Kwa ajili yao wanaoteseka wenye njaa, hofu, wasio na haki, na wenye kukandamizwa=

Kwa ajili yao walio hatarini, wenye huzuni, au matatizo ya aina yoyote
=Kwa ajili yao watoao huduma kwa wagonjwa, wasio na marafiki, na wahitaji=

Kwa ajili ya amani na umoja wa kanisa la Mungu
=Kwa ajili yao wote waitangazao injili, na hao waitafutayo kweli=

Kwa ajili ya Randolph Baba na Mwanzilishi wetu, Dale Askofu wetu Mkuu, na Philip Askofu msaidizi wake na maaskofu wote pamoja na wachungaji
=Kwa ajili yao wote watoao huduma katika kanisa la Mungu

Waumini wanakaribishwa kuongeza maombi yako binafsi

Utusikie; Ewe Bwana;
=kwa kuwa fadhili zako ni kuu

Tunakushukuru, Bwana, kwa baraka zote katika maisha haya.
Waumini wanakaribishwa kuongeza shukrani zao binafsi

Tutakuinua wewe, Ewe Mungu Mfalme wetu
=Na kulisifu Jina lako milele na milele=

Tunaomba kwa ajili yao waliofariki dunia katika imani ya kweli, ili wadumu katika ufalume wako milele.

Waumini wanakaribishwa kuongeza maombi yao
Bwana utuletee upendo-na ukarimu wako kwetu
=Ambao kwako tumeweka imani yetu =

Mhudumu atamaliza kwa sala

MAUNGAMO YA DHAMBI

Shemasi au Mhudumu: Na tumuungamie Mungu Mkuu dhambi zetu, kwa kutumia taratibu

_____

Waumini wakiwa wamepiga magoti, wote waseme moja ya ungamo ifuatavyo

1.) Ewe Mungu mwenye enzi, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, muumba vitu vyote, mhukumu watu wote: Twaungama na kuzililia dhambi zetu na uovu wetu ambao tumefanya mara kwa mara kwa mawazo, maneno, na matendo kinyume chake yeye mtakatifu na mtawala wetu, tumewasha hasira yako ya hakika na chuki kinyume chetu. Tunatubu sana na tunasikitika toka mioyoni mwetu kwa ajili ya matendo yetu haya. Tukikumbuka tuna huzuni, na mzigo wake hauchukuliki. Tuhurumie, tuhurumie wewe Baba mwenye huruma, kwa ajili ya mwanao Bwana wetu Yesu Kristo tusamehe kwa yote ya kale na utujalie tukutumikie katika upya wa maisha yetu kwa ajili ya heshima na utukufu wa jina lako; kwa ajili yake Yesu Kristo Bwana wetu, Amina.

1.) Baba Mwenye enzi mwenye huruma, tumekosa na kutawanyika kama Kondoo waliopotea. Tumefuata sana mawazo yetu na tamaa za mioyo yetu. Tumezihalifu sheria zako takatifu. Tumeacha kufanya yale yatupasayo kutenda na tumefanya yale yasiyotupasa kutenda. Tunasikitika kweli na kutubu kwa unyenyekevu. Lakini wewe Bwana, utujalie huruma yako waachilie hao wanaotubu dhambi zao, na uwasamehe hao walio na toba la kweli, kufuatana na ahadi zako ulizozitoa kwa wanadamu katika Yesu Kristo Bwana wetu; Utujalie ewe Baba mwenye huruma, kwa ajili yako tuishi Kiuungu, kwa haki, na usafi wa maisha kwa ajili ya jina lako takatifu. Amina..
2. 3.) Baba mwenye rehema nyingi, twaungama kwamba
3. tumekukosea wewe kwa mawazo, maneno, na matendo, kwa yale tuliyoyafanya na kwa yale ambayo tumeacha bila kufanya. Tumeshindwa kukupenda wewe kwa mioyo yetu yote, tumeshindwa kuwapenda marafiki zetu kama nafsi zetu. Tunasikitika sana na tunatubu kwa sababu ya machungu ya kukosa furaha ya peponi na kupata maumivu ya jehanamu; lakini zaidi sana ni kwa sababu ya kukukosea wewe, Mungu wetu, wewe ambaye ni mwema na unayestahili upendo wetu wote.
4. Kwa hiyo, kwa ajili ya mwanao Yesu Kristo, utuhurumie na utusamehe; ili tuendelee kufurahi katika katika mapenzi yako, na kutembea katika njia zako kwa ajili ya utukufu wa jina lako. Amina.
5.
6. *Askofu, Akiwepo, au Mchungaji husimama na kutoa ondoleo la dhambi, akifanya alama ya msalaba kwa waumini.*
7. Bwana mwenye enzi na mwenye huruma awajalie msamaha na ondoleo la dhambi zenu zote, awajalie ungamo l a kweli, maisha ya utakaso, neema, na faraja ya Roho wake Mtakatifu. Amina.
8.
9. *Au hivi:*
10.
11. Ewe mwenyezi Mungu, Baba wa mbinguni, wewe ambaye kwa neema yako umeahidi ondoleo la dhambi kwa wale wote wakujiao kwa toba na imani ya kweli, akuhurumieni, akusameheni, akuokoeni kutoka katika dhambi zenu zote akuhakikishieni na kukutieni nguvu katika mema yote na kukuleteeni maisha ya milele kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo. Amina
12.
13. *Au hivi:*

14.
15. Mwenyezi Mungu kurehemuni, akusameheni dhambi zenu kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo, akutieni nguvu na mema yote na nguvu za Roho wake Mtakatifu awaweke katika uzima wa milele. Amina.
16.
17. **AMANI**
18. *Wote wasimame:*
19. *Mhudumu aseme kwa watu*
20. Amani ya Bwana iwe pamoja nanyi siku zote.
21. **Waumini:** Iwe nawe pia
22.
23. *Wahudumu na waumini waweza kusalimiana kila mmoja katika jina la Bwana.*
24.
25. **SADAKA**
26. *Moja ya sentensi hii yaweza kutumika:*
27.
28. Mpeni Mungu utukufu sawasawa na jina lake; leteni sadaka na mje katika nyua zake.
29.
30. Tembeeni kwa upendo kama Kristo alivyotupenda na kujitoa nafsi yake kwa ajili yetu, toleo na sadaka safi na yenye mapenzi mema kwa Mungu.
31.
32. Nawasihini sasa enyi watakatifu, kwa rehema za Mungu ili mulete miili yenu kama sadaka ya maisha, matakatifu, na inayopokeleka kwa Mungu kama huduma kamilifu.
33.
34. **MATOLEO YA ZAWADI**

Utukufu una Mungu juu mbinguni

Mhudumu anainua fungu la kumi na sadaka, mkate, na divai kwa kupokezana na kusema ifuatanyo:

Mhudumu: Ubarikiwe ewe Mungu baba wa maumbile yote, katika wema wako tunayo haya mafungu pamoja na sadaka ambayo ni ishara ya maisha na kazi zetu; na vitumike katika kanisa lako kwa kazi uliyoiweka mbele yetu na kwa kuendeleza ufalme wako.

Waumini: Ubarikiwe Mungu Milele

Mhudumu: Ubarikiwe wewe, Bwana Mungu wa viumbe vyote.
Tunakutolea mkate huu kwa ajili ya wema wako
Zao la dunia hii na kazi ya mikono yetu;
Mkate huu uwe kwetu mwili wa Kristo

Waumini: Ubarikiwe Mungu Milele

Mhudumu: Wewe Bwana Mungu wetu, tunapochanganya maji na divai hii ni kito cha ushirika wa uungu na asili ya kibinadamu ya Yesu Kristo, tunaonywea kikombe

hiki na tushiriki katika uungu wa kristo ambaye yeye mwenyewe alijinyenyekeza kushiriki katika ubinadamu wetu.

Waumini: Amina

Mhudumu: Ubarikiwe wewe, Bwana Mungu wa viumbe vyote.
Kwa ajili ya wema wako tunakutolea divai hii, tunda la mzabibu Na kazi ya mikono yetu binadamu; divai hii iwe kwetu damu ya Kristo

Waumini: Ubarikiwe Mungu Milele

Mhudumu: Natuombe, ndugu zangu, ili sadaka yetu iweze kupokelewa kwa Mungu, Baba mwenye enzi.

Waumini: Mungu na apokee sadaka hii iliyo katika mikono yako kwa ajili ya sifa na utukufu wa jina lake, kwa ajili ya mema juu yetu na wema wa kanisa lake lote.

SHUKRANI KUU

Watu wabaki wamesimama na mhudumu awaelekee na kusema:

Mhudumu: Mungu awe nanyi
Waumini: Awe pia na roho yako
Mhudumu: Inueni mioyo yenu
Waumini: Twaiinua kwa Bwana
Mhudumu: Na tumshukuru Bwana Mungu wetu
Waumini: Ni haki kumshukuru na kumtukuza

Mhudumu andelee na maneno haya:

Ni jambo la haki, jema na la furaha kuu, wakati wote na kila mahali kumshukuru Mungu, Baba mwenye enzi muumba wa mbingu na dunia.

MANENO SAHIHI YA UTANGULIZI YAINGIZWE HAPA

Mhudumu aendelee

Kwa hiyo, tunakusifu wewe, tukiunganisha sauti zetu na malaika, na makerubi pamoja na jeshi lote la mbinguni ambao milele huimba wimbo huu wa kutangaza utukufu wa jina lako.

Mtakatifu wa Watakatifu

Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu Bwana, Mungu mwenye nguvu na mwenye enzi,
Mbingu na nchi zimejaa utukufu wako.
Hosana palipo juu.
♋ Abarikiwe yeye ajaye katika jina la Bwana.
Hosana palipo juu.

Ushirika Mtakatifu A

Waumini wasimame au wapige magoti. Mhudumu aendelee:

Bwana Mtakatifu na mwenye Rehema: Kwa upendo wako usio na kikomo ulituumba kwa ajili yako, na tulipokuwa tumeanguka katika dhambi na kuwa watumwa wa dhambi na mauti, wewe kwa huruma yako ulimleta Yesu Kristo, mwana pekee wa milele kushiriki asili yetu ya ubinadamu, kuishi na kufa kama mmoja wetu, kutupatanisha na wewe Mungu, Baba wa wote. Alitandaza mikono yake msalabani, na kujitoa mwenyewe, kwa kutii mapenzi yako, sadaka kamili kwa dunia yote

Katika maneno yafuatayo, mhudumu ashikilie au aweke mikono juu yake; na kwa maneno yahusianayo na kikombe; ashikilie au kuweka mkono juu ya kikombe na viriba vinginenvyo vyenye divai kwa ajili ya wakfu.

Na kwa hiyo, Baba, ambao tumeokolewa naye na kufanywa viumbe wapya kwa maji na kwa Roho Mtakatifu, sasa tunakuletea zawadi hizi. ☩ zitakase kwa Roho wako mtakatifu ziwe mwili na damu ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Yeye usiku ule aliotolewa kwa mateso na kifo, Bwana wetu Yesu Kristo alitwaa mkate; na akiisha kukushukuru, aliumega na akawapa wanafunzi wake akisema, “Twaeni mle: Huu ni mwili wangu , uliotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi.”

Baada ya chakula alitwaa kikombe cha divai; na alipokuwa ameshukuru, aliwapa wanafunzi wake akisema, “Nyweeni katika hiki ninyi nyote: Hii ni damu yangu ya agano jipya, ambayo iliemwagika kwa ajili yenu na kwa wengi kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Fanyeni hivi kila mywapo kwa kunikumbuka mimi.”

Kwa iyo tunatangaza maajabu ya imani
Mhudumu na Waumini

Kristo Amekufa
Kristo Amefufuka
Kristo atakuja tena

Mhudumu anaendelea

Tunashangilia kumbukumbu la wokovu wetu, Ee Baba, kwa sadaka na shukrani. Tukikumbuka kifo chake, ufufuo, na kupaa kwake, tunatoa zawadi hizi.. ☩ Zitakase kwa Roho wako Mtakatifu ili kwa watu wako ziwe mwili na damu ya mwanao Yesu, chakula kitakatifu, kinywaji kipya na maisha yasiyo na kikomo kwake. Tutakase pia ili kwa uaminifu tuweze kupokea sakramenti yako takatifu, na tukutumikie katika umoja, kiasi, na amani; na siku ya mwisho utulete pamoja na watakatifu wako katika furaha ya ufalme wa mbinguni. Tunaomba haya yote kwa kupitia jina la mwanao Yesu Kristo: Kwa yeye, na katika yeye na ndani ya yeye kwa umoja wa Roho Mtakatifu heshima na utukufu ni wako, Baba mwenye enzi, sasa na hata Miele. Amina.

Ushirika Mtakatifu B

Watu wasimame au wapige magoti. Mhudumu aendelee:

Utukufu uwe kwako ewe mwenyezi Mungu, Baba wa mbinguni ambaye kwa rehema zako za kweli, ulimtoa mwana wako pekee Yesu Kristo afe pale msalabani kwa ajili ya wokovu wetu; yeye ambaye alifanywa, kuwa kafara moja alijitoa mwenyewe sadaka kamili, ya hakika, na ya kutosha, kafara inayotosha kwa ajili ya dhambi za dunia yote, mwenye kuanzisha, na katika injili yake kutuamuru kuendelea kumbukumbu kifo na sadaka hadi atakoapo kuja tena.

Katika maneno yafuatayo katika kuumega mkate mhudumu ashikilie au awekee mikono juu yake; na kwa maneno yahusianayo na mkate; ashikilie au kuweka mkono juu ya kikombe na viriba vinginenvyo vyenye divai kwa ajili ya wakfu

Na kwa hiyo, Baba, sisi ambao tumeokolewa na yeye, na kufanywa watu wapya kwa maji na kwa Roho Mtakatifu, sasa tunakuletea zawadi zetu. 𝕀 Zitakase kwa Roho wako Mtakatifu ili ziwe mwili na damu ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Yeye usiku ule aliosalitiwa, alitwaa mkate, na alipokuwa ameshukuru, aliumega, na akawapa wanafunzi wake akisema, "twaeni mle, huu ndio mwili wangu, ambao umetolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi."

Vivi hivi, baada ya kula jioni, alitwaa kikombe, na akisha kushukuru aliwapa wanafunzi wake akisema, "Kunyweni hii; ndiyo damu yangu ya agano jipya ambayo imemwagwa kwa ajili yenu na kwa wengi kwa ondoleo la dhambi. Fanyeni hivi, kila mnywapo kwa ukumbusho wangu."

Kwa hiyo, ewe Bwana, Baba wa mbinguni, kufuatana na kanuni ya mwanao mpendwa Yesu Kristo, watumishi wako wanyenyekevu, tunashangilia na kufanya mbele zako wewe mwenye uungu mkuu, kwa hizi zawadi takatifu ambazo tunakutolea wewe, kumbukumbu ambayo mwanao mpendwa ametuagiza kufanya; katika kukumbuka baraka za mateso yake makuu, kifo chake cha thamani, ufufuko wake wa enzi na utukufu wa kupaa kwake; akikuletea shukrani za rohoni na fidia iliyokamilika ya kututwaa . Na kwa unyenyekevu wote tunatafuta uso wako, ewe Baba mwenye huruma, ili utusikie, na kwa wema wako mkuu, tukae kwa salama na baraka 𝕀 na utakaso, kwa neno lako na kwa Roho wako Mtakatifu, sadaka hizi na viumbe ambavyo ni mkate na divai; ambayo tunapokea kufuatana na kanuni za mkombozi wetu Yesu Kristo, kwa kumbukumbu za kifo chake, na mateso yake ili tuwe washiriki wa mwili na damu yake yenye baraka tele.

Na tunatamani kwa undani ewe Baba yetu mwema na mwenye rehema, upokee hii sadaka ya sifa na shukrani; zaidi kwa unyenyekevu tukikuomba utujalie hivi kwa heshima ya kifo cha mwanao Yesu Kristo kwa imani ya damu yake, pamoja na kanisa lake lote tuweze kupata ondoleo la dhambi zetu na fidia yote ya mateso yake.

Na sasa wewe Bwana, tunajitoa na kukuletea nafsi zetu, roho zetu, na miili yetu ili iwe sadaka kamilifu, takatifu na ya kudumu kwako. Tunatafuta kwa unenyekevu kwamba pamoja na wengine wengi tuwe washiriki wa ushirika huu, ili tuthamini kupokea mwili wenye thamani kuu

na Damu ya mwanao Yesu Kristo, tujazwe neema yako na baraka zako za mbinguni na tufanywe mwili mmoja na yeye ili akae ndani yetu nasi ndani yake. Ingawa hatustahili chochote kwa ajili ya dhambi zetu, kutoa sadaka mbele zako ewe mwenyezi Mungu, tungali twakuomba upokee majukumu yetu na kujitahidi kwetu, si kwa kupima kustahimili kwetu bali kwa kutusamehe makosa yetu. Kwa ajili yake Yesu Kristo aliye Bwana wetu;

Ambaye kwake, katika yeye, na ndani ya umoja wa Roho Mtakatifu, heshima yote na utukufu uwe kwake, Baba mwenye enzi ulimwengu usiyo na kikomo. Amina.

Ushirika Mtakatifu C:

Watu wasimame au wapige magoti
Ndipo mhudumu aendelee

Tunakutolea shukrani wewe, ewe Mungu, kwa wema wako na upendo wako ambao unadhihirika katika maumbile yako; katika kuwaita Israel wawe watu wako; katika maneno yako kupitia vinywa vya manabii, na zaidi ya yote, katika neno aliyefanyika mwili, Yesu mwana wako. Na katika siku hizi za mwisho ulimtuma atungwe mimba na bikira Mariamu, mwokozi na mkombozi wa dunia. Katika yeye, umetuokoa kutoka katika mabaya na kutufanya wa thamani mbele zako. Katika yeye umetutoa makosa na kutuleta katika kweli, katika dhambi na kuwa wenye haki, katika mauti hadi uzima.

Katika maneno yafuatayo, mhudumu ashikilie au awekee mikono juu yake; na kwa maneno yahusianayo na kikombe; ashikilie au kuweka mkono juu ya kikombe na viriba vinginenvyo vyenye divai kwa ajili ya wakfu

Na kwa hiyo, Baba, ambao tumeokolewa na yeye, na kufanywa watu wapya kwa maji na kwa Roho Mtakatifu, sasa tunakuletea zawadi zetu. 亚 Zitakase kwa Roho wako Mtakatifu ili ziwe mwili na damu ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Usiku ule kabla hajafa kwa ajili yetu Bwana Yesu Kristo aliutwaa mkate, na alipokuwa ameshukuru, aliumega, na akawapa wanafunzi wake akisema, “twaeni mle, huu ndio mwili wangu, ambao umetolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi.”
Baada ya chakula, alitwaa kikombe, na akisha kushukuru aliwapa wanafunzi wake akisema, “ Nywweni katika hiki; hii ni damu yangu ya agano jipya ambayo imemwagwa kwa ajili yenu na kwa ajiliya wengi kwa ondoleo la dhambi. Fanyeni hivi, kila mnywapo Kwa ukumbusho wangu.”

Kama mlivyoagizwa na Baba

Mhudumu na Waumini

Tunakumbuka kifo chake
Tunatangaza kufufuka kwake
Tunanatazamia kurudi kwake kwa utukufu

Mhudumu aendelee

Na sasa tunatoa sadaka zetu za sifa na shukrani kwako wewe Bwana wa wote; tukikuletea mazao ya viumbe vyako, mkate huu na divai hii. Tunaomba kwako wewe Mungu mwenye rehema, utushushie roho wako mtakatifu katika zawadi zetu ili ziwe sakramenti ya mwili ☩ wa Kristo na damu ☩ ya agano jipya. Utuunganishe na sadaka ya mwanao, ili tuweze kupokeleka kwa kupitia kwake, kwa utakaso wa Roho wako Mtakatifu. Na kwa mda kamili, uweke vitu vyote katika ulinzi wa Kristo, na utulete katika inchi ile ya mbinguni ambapo, pamoja (N) watakatifu tuweze kuingia katika urithi wa milele pamoja na wana wako na mabinti zako; kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu, mzaliwa wa kzwanza wa viumbe vyote, mkuu wa kanisa, na mwanzilishi wa wokovu wetu.

Ambaye kwake yeye, katika yeye, na ndani ya umoja wa Roho Mtakatifu, heshima yote na utukufu uwe kwake, Baba mwenye enzi ulimwengu usiyo na mwisho. Amina.

Ushirika Mtakatifu D:

Watu wasimame au wapige magoti
Ndipo mhudumu aendelee

Tunakutangaza wewe, Baba mtakatifu, Mtukufu mwenye nguvu.
Kazi zako kuu zinadhihirisha hekima na upendo wako. Ulituumba sis kwa mfano wako, na kutupa dunia yote chini ya ungalizi wetu, ili katika kukutii, wewe muumbaji wetu tuweze kutawala na kuhudumia viumbe vyote.

Wakati kutokutii kwetu kulipotufarakanisha na wewe, hukutuacha katika nguvu za mauti, kwa rehema zako ulikuja utuokoe ili katika kukutafuta wewe tupate kukuona. Tena na tena ulituita katika agano na Wewe, na kwa njia ya manabii ulitufundisha tuwe na matumaini ya wokovu.

Baba, uliupenda ulimwengu sana kiasi kuwa katika mda ulio kamilika, ulimtuma mwanao pekee awe mkombozi wetu. Aliyetungwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, akazaliwa na bikira Mariamu, Akaishi kati yetu, bali bila dhambi. Kwa maskini alitangaza habari njema za wokovu; kwa wafungwa, uhuru; kwa wenye huzuni, furaha. Kukamilisha makusudi yako alijijitoa nafsi yake hadi mauti; na kwa kuinuka kutoka kaburini aliyashinda mauti, na kufanya viumbe vyote upya.

Katika maneno yafuatayo katika kuumega mkate mhudumu ashikilie au awekee mikono juu yake; na kwa maneno yahusianayo na mkate; ashikilie au kuweka mkono juu ya kikombe na viriba vinginenvyo vyenye divai kwa ajili ya wakfu

Mungu tunaomba kwamba, katika wema wako na rehema zako Roho wako Mtakatifu azishukie zawadi hizi ☩ zitakase ewe Bwana, ukizionyasha kuwa sadaka takatifu kwa watu wako watakatifu, mkate wa uzima, na kikombe cha wokovu, mwili na damu ya mwana wako Yesu Kristo. Mungu tujalie kwamba wote wanaoshiriki katika mkate mmoja na kikombe kimoja wawe mwili mmoja na roho moja, ☩ sadaka iliyo hai kwa Kristo na kwa sifa ya jina lako.

Wakati saa ilipotimia kwa yeye kutukuzwa na wewe, Baba yake wa mbinguni, aliewapenda walio wake ambao walikuwa duniani, aliwapenda hadi ukamilifu wa dahari.

Akiwa mezani pamoja nao Bwana Yesu alitwaa mkate, na akisha kushukuru, aliumega na kuwapa wanafunzi wake nakusema, "Twaeni mle: Huu ni Mwili wangu ambao umetolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kila mlapo kwa ukumbusho wangu."

Baada ya chakula, alitwaa kikombe cha divai, na akisha kushukuru, akawapa wanafunzi wake akisema, "Nyweeni katika hiki ninyi nyote. Hii ni damu yangu ya agano jipya ambayo imemwagwa kwa ajili yenu na kwa wengi kwa ondoleo la dhambi. Fanyeni hivi kila mywapo kwa ukumbusho wango."

Kwa hiyo, ewe baba, tunatangaza maajabu ya imani yetu

Mhudumu na Waumini

Tunakumbuka kifo chake
Tunatangaza kufufuka kwake
Tunanatazamia kurudi kwake kwa utukufu

Mhudumu aendelee

Baba, sasa tunashangilia kumbukumbu hii ya ukombozi wetu.
Tukikumbuka kifo cha Yesu na kushuka kuzimu,
Tukitanganza kufufuka kwake na kupalizwa katika mkono wako wa kuume Tukitazamia kurudi kwake kwa utukufu, na kutoa kwako mwili na damu yake sadaka inayokubalika nawe na wokovu wa ulimwengu mzima.

Kumbuka ewe Bwana, kanisa lako takatifu na apostoliko, lililokombolewa kwa damu ya Yesu, Kristo mwana wako. Funua umoja wake, ongoza imani yake, na tunza amani yake. Kumbuka wale ambao kwao tunatoa sadaka hizi na hasa Randolph, Baba Mwanzilishi wetu na Askofu wetu mkuu. Dale Askofu Mkuu wa Jimbo letu; na Philip msaidizi wa Askofu.

Na wote watoao huduma katika kanisa lako. Wakumbuke watu wako wote, na wote wanaotafuta kweli yako.

Wakumbuke wote walifariki katika amani ya Kristo na hao ambao imani zao zinajulikana kwako wewe; walete katika sehemu ya furaha na mwanga wa milele.

Tujalie ewe Baba mwenye rehema, ili tuweze kupata urithi wetu pamoja na mbarikiwa Bikira Mariamu, mama wa Mungu, pamoja na Mtakatifu Yusufu, mababa wa imani, manabii, mitume, na mashahidi (na N) na watakatifu wote ambao wamepata kibali machoni pako katika miaka iliyopita. Tunakusifu wewe kwa kushirikiana nao na kukukupa utukufu kupitia kwa mwanao Yesu Kristo Bwana wetu.

Kwa njia ya Kristo, katika Kristo na ndani ya Kristo, heshima zote na utukufu zina wewe mwenye enzi Mungu na Baba, kwa umoja wa Roho Mtakatifu, sasa milele na milele. Amina.

SALA YA BWANA

Na sasa kama mwokozi Yesu Kristo alivyotufundisha , tunathubutu kusema
Waumini na Mhudumu
Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe
Ufalme wako uje, mapenzi yako yatumizwe, hapa duniani
Kama huko mbinguni, utupe leo mkate wetu wa kila siku
Na utusamehe makosa yetu, kama nasi tunavyowasamehe
wale waliotukoesea. Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule
mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu na utukufu hata milele. Amina

Kuumega Mkate

Mhudumu anamega mkate uliowekwa wakfu
Hapa kunakuwa na kipindi cha ukimya.

Halafu panaweza kuibwa au kusema

{Haleluya} Yesu pasaka wetu amekwisha kutolewa kwetu;
=kwa hiyo na tusherehekee karamu yetu. { Halelueya }

Wakati wa mafungo, haleluya huachwa na pia inaweza kuachwa nyakati zingine isipokuwa wakati wa Kwaresma.

Akiwaelekea watu, mhudumu awakaribishe waumini ifuatavyo:

Zawadi ya Mungu kwa watu wa Mungu.

Pia anaweza kuongeza.

Utwae kwa kumbukumbu kuwa Kristo alikufa kwa ajili yako, mleni yeye miononi mwenu kwa shukrani.

Wahudumu wanapokea sakramenti kwa namna zote na mara moja wanatoa kwa waumini.

Mkate na kikombe vinatolewa kwa washiriki kwa maneno haya:
Mwili (damu) ya Bwana wetu Yesu Kristo ikulinde hata uzima wa milele. [= Amina. =]

Au kwa maneno haya
Mwili wa Kristo, Mkate wa mbinguni. [Amina]
Damu ya Kristo, kikombe cha wokovu. [Amina]

Wakati wa huduma ya ushirika mtakatifu, nyimbo, zaburi, au za utaifa zinaweza kuimbwa Kuwapo na ulazima, kiongozi wa ibada ataweka wakfu mkate na divai akitumia maombi yaliyo mwisho wa ibada hii.

Baada ya ushirika, mhudumu aseme:

Na tuombe
Mhudumu na Waumini

I. Mungu wa milele, Baba wa mbinguni, kwa neema yako umetupokea kama jamii iliyo hai ya mwanao Yesu Kristo, na umetulisha chakula cha rohoni katika sakramenti ya mwili wake na damu yake. Ututume sasa ewe Mungu duniani kwa amani yako, na utujalie nguvu na moyo wa kukupenda na kukutumikia wewe kwa shukrani na upya wa maisha yetu; kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu. Amina

Au ifuatayo

I. Mwenye enzi na Mungu uishie milele, tunakushukuru kwa kutulisha chakula cha kiroho kwa mwili cha mwili wenye thamni na damu ya mwanao mpendwa Yesu Kristo; na kutuhakikishia katika maajabu haya kuwa ni viumbe hai wa jamii ya mwili wa mwanao, na warithi wa ufalme wako wa milele. Na sasa, Baba, ututume tukafanye kazi uliyotutuma, kukupenda nakukutumikia wewe kama mashahidi waaminifu wa Yesu Kristo. Kwake yeye, kwako, na kwa Roho Mtakatifu, heshima na utuhufu sasa na hata milele. Amina.

Askofu, akiwepo, au mchungaji, anaweza kuwabariki waumini

Amani ya Bwana, ipitayo fahamu zote, iwalinde mioyo yenu, na akili zenu, katika fahamu na upendo wa Mungu na mwanae Yesu Kristo Bwana wetu; na baraka za mungu mwenye enzi, Baba, ☩ Mwana, na Roho Mtakatifu ziwe nayi, zikae nanyi daima. Amina.

Ka au mhudumu, awaage watu kwa kusema maneno haya

Na tuende kwa jina la Yesu
Waumini: Shukrani ziwe kwa Mungu

Au hivi
Kasisi: Enendeni kwa amani, mkampende na kumtumikia Mungu
Waumini: Shukrani ziwe kwa Mungu

Au hivi
Kasisi: Na tuenende duniani , tukifurahi katika nguvu za Roho mtakatifu
Waumini: Shukrani ziwe kwa Mungu

Au hivi
Kasisi: Na tumbariki Mungu wetu
Waumini: Shukrani ziwe kwa Mungu

Kama mkate uliowekwa wakfu au divai haivitoshelezi washiriki, mhudumu anapaswa kurudi katika meza takatifu na kuweka wakfu moja au vyote, kwa kusema

Tusikie ewe Baba wa mbinguni na kwa Neno lako na Roho Mtakatifu na takasa 丌 mkate huu (divai) ili pia iwe sakramenti ya mwili wako wa thamani (damu) ya (wako) mwanao Yesu Kristo Bwana, ambaye alichukua 丌 mkate (kikombe) na kusema
“ huu ni mwili wangu (Damu).” = Amina=